**HOTUBA YA MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE SHEREHE ZA MIAKA 60 YA KUANZISHWA KWA ATE, TAREHE 3 DESEMBA, 2020**
**HOTELI YA SERENA, DAR ES SALAAM**

## SALAMU

- Bi. Jayne Nyimbo, Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE),
- Mhe. Alhaji Abubakari Kunenge – Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,
- Mwakilishi wa Ubalozi wa Norway – Tanzania,
- Mwakilishi wa KM – OWM – Kazi na Ajira, Bwana Kadugusi,
- Bw. Wellington Chibebe, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa nchi za Tanzania, Kenya, Rwanda, Uganda na Burundi,
- Bw. Felix Kagisa, Makamu Mwenyekiti wa ATE,
- Wajumbe wa Bodi - mpya na ya zamani,
- Dkt. Aggrey K. Mlimuka, Mkurugenzi Mtendaji na Afisa Mtendaji Mkuu wa ATE,
- Waheshimiwa Wabunge- Namtambua Mheshimiwa Maige,
- Bw. Saidi Wamba, Kaimu Katibu Mkuu TUCTA,
- Mheshimiwa Abood Jaji wa Mahakama Kuu idara ya Kazi,
- Wageni Waalikwa,
- Waandishi wa Habari,
- Mabibi na Mabwana.

**Habari za asubuhi !**

## SHUKRANI NA PONGEZI

**Ndugu Mwenyekiti,** awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kufika siku hii ya leo kushuhudia maadhimisho ya miaka 60 ya Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa kunikaribisha kuungana nanyi kuwa Mgeni Rasmi wa tukio hili muhimu sana la maadhimisho ya miaka 60 ya kuanzishwa kwa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Zaidi ya hayo, napenda kuwashukuru ATE hasa wanachama wake wote wanaotoka katika Sekta zote za Uzalishaji kwa mchango wenu mkubwa katika kukuza na kuboresha uchumi wa taifa letu na kuwezesha nchi yetu kupanda kutoka kuwa taifa la uchumi wa chini mpaka kuwa Taifa la Uchumi wa Kati tangu Mwezi Julai Mwaka huu.

**Ndugu Mwenyekiti,** kabla sijaendelea na hotuba yangu, naomba mpokee salamu za pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa pamoja na Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais. Viongozi wetu hao, wanawapa pongezi nyingi sana kwa kufanikisha maadhimisho haya ya miaka 60 ya kuanzishwa kwa ATE.

**Ndugu Washiriki,** wakati ATE inafikisha miaka 60 mwaka huu, ifikapo tarehe 9 Disemba, Nchi yetu itakuwa inaadhimisha miaka 59 ya Uhuru na miaka 58 ya Jamhuri; Kaulimbiu yetu kwa mwaka huu ni: **"Tanzania yenye uchumi imara itajengwa na Watanzania wenyewe."**

**TUFANYE KAZI KWA BIDII, UWAJIBIKAJI NA UADILIFU**

Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameagiza maadhimisho ya sherehe za Uhuru mwaka huu yafanyike kwa kufanya shughuli mbalimbali za Kijamii. Aidha, Fedha, **shilingi milioni 835,498,700/=** zilizokuwa zitumike kwa maadhimisho ya sherehe na burudani zitumike kukamilisha shughuli za umaliziaji hospitali ya UHURU jijini Dodoma.

Ujenzi wa Hospitali ya Uhuru Mkoani Dodoma in utekelezaji wa Agizo la Mhe. Rais, alilolitoa Novemba, 2018 ambapo:-

i. Aliagiza **shilingi milioni 995,182,100/=** zilizokuwa zimetengwa kwa maadhimisho ya miaka 57 ya uhuru wa Tanzania Bara zitumike kwa ujenzi wa Hospitali hii;
ii. Aidha, mwezi Januari, 2019 Mhe. Rais, wakati anapokea gawio la hisa za kampuni ya simu ya AIRTEL aliagiza **shilingi bilioni 2.4 (2,415,151,650/=)** pia, zitumike kwa ujenzi wa hospitali hii;

**Ndugu Mwenyekiti,** tarehe 20 Novemba, 2020 nilitembelea hospitali hii na kukuta ujenzi umefikia asilimia 92. Kazi zilizokuwa zimebaki ni uwekaji tiles, ceiling board, gypsum,upigaji rangi, uwekaji milango na mifumo ya maji safi na taka;

**Ndugu Mwenyekiti,** ujenzi mpaka sasa zimetolewa shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya jengo la ghorofa moja lenye maeneo yafuatayo:-

i. Wagonjwa wa nje (OPD);
ii. Kliniki ya Mama na Mtoto;
iii. Matibabu ya Kinywa na Meno;
iv. Matibabu ya Masikio, Pua na Koo;
v. Matibabu ya Macho;
vi. Maabara;
vii. Mionzi;
viii. Utawala.

Hata hivyo, Hospitali hii tumeijenga mita 200 kutoka barabara kuu;

**Ndugu Mwenyekiti,** tarehe 29, Juni 2020, Halmashauri iliomba Hazina **shilingi bilioni 1.039 (1,039,000,000/=)** kwa ajili ya umaliziaji, dawa, ununuzi wa samani na vifaa vya ofisini, vifaa tiba, vifaa vya maabara, uzio, n.k.

**Ndugu Mwenyekiti**, kipekee kabisa napenda kutumia muda huu kuwapongeza ATE kwa kutimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. Sote tunafahamu kwamba ATE ilianzishwa mnamo mwaka 1960 kipindi kabla ya uhuru wa Tanganyika ikijulikana kama Shirikisho la Waajiri wa Tanganyika na imeendelea kudumu hadi sasa. Niwapongeze sana kwa kukabiliana na changamoto mbalimbali na kwa kazi nzuri mliyoifanya na mshikamano mlio nao ambao umekuwa chachu ya kuendelea kuwepo na kuwatumikia watanzania hadi leo kufikisha umri wa miaka 60. **HONGERENI SANA**.

**KAULI MBIU YA MAADHIMISHO YA MIAKA 60 YA ATE**

Nimefurahi sana kuona maadhimisho haya yakienda sambamba na mada inayosema: **"Uchumi wa kati endelevu unaotokana na mazingira bora ya biashara na maendeleo ya ujuzi Tanzania."** Kama mnavyofahamu hivi karibuni Tanzania imefanikiwa kuingia katika nchi zenye kipato cha uchumi wa kati huku suala la kuendeleza ujuzi likiendelea kuwa kiungo muhimu katika kufikia hatua hii kubwa kiuchumi.

Serikali inatambua umuhimu wa kuweka mazingira bora katika kukuza uchumi wetuna kupitia Ilani ya CCM ya 2020 imepanga kuweka mazingira wezeshi ya biashara, kuhakikisha upatikanaji wa fursa nafuu za biashara ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kaulimbiu hii inahimiza umuhimu wa kuendeleza ujuzi katika kuimarisha uchumi wa kati ambalo ni suala la msingi kabisa. Napenda kuwahakikishia kwamba Serikali inatambua mchango wa Chama cha Waajiri Tanzania katika kukuza ujuzi na kuhamasisha waajiri kuwekeza katika usimamizi mzuri wa Rasilimali watu kama moja ya nyenzo muhimu za kukuza uchumi wetu.

Ninafahamu ATE kwa sasa inashirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kutekeleza mpango wenye lengo la kuongeza uelewa miongoni mwa Waajiri nchini kuhusiana na umuhimu wa Uanagenzi pamoja na programu nyingine za mafunzo mahala pa kazi kwa wahitimu ili kuongeza fursa za Ajira hasa kwa vijana wenye sifa za kuajirika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ni vema wote tukatambua kwamba, suala la kuendeleza ujuzi ni moja ya kipaumbele kilichopo katika Dira ya Taifa ya maendeleo ya 2025. Pia ifahamike kuwa serikali sasa imekamilisha awamu ya kwanza ya kutekeleza mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na sasa ikiwa ni Awamu ya Pili ambao unalenga kuongeza idadi ya watu wenye ujuzi wa kutosha kama kiungo muhimu katika ukuaji wa uchumi wetu na ustawi wa jamii nzima.

Niwatake waajiri wote nchini muendelee kuunga mkono juhudi hizi za kuendeleza ujuzi kwa kuwapatia fursa Vijana wetu wanaotoka katika taasisi mbalimbali za elimu kuweza kujifunza katika maeneo yenuya kazi kwani hii itasaidia sana kutengeneza Taifa lenye Vijana wengi wenye ujuzi kwa manufaa ya nchi yetu.

Kwa mara nyingine niwapongeze kwa kauli mbiu yenu ambayo imesawiri kwa kiasi kikubwa hali na mahitaji halisi ya nchi yetu katika kipindi hiki ambacho nchi yetu imeshaingia katika uchumi wa kati.

**MKAKATI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO KUBORESHA MAZINGIRA YA BIASHARA NA UWEKEZAJI**

**Kuondoa Utitiri wa kodi**:

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Leo nimefurahi kupokea wasilisho la mwendo wa kiuchumi kutoka kwa Dkt. Mmari**,** Serikali inatambua changamoto mbalimbali ambazo waajiri wameendelea kukumbana nazo ikiwemokuhusu **utitiri wa kodi.** Kwa kutambua hilokupitia Ilani ya CCM 2020/2025 imesisitizwa kuimarisha utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini (**Bleuprint for Regulatory Reforms to improve the Business Environment**).

Katika miaka mitano iliyopita tumefanikiwa kuweka mkazo kwenye sekta zinazoleta Makubwa, Biashara, Kikao Mifugo, uvuvi na tunaanza kuimarisha kufuta tozo **168** ambapo 114 zilihusu sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi huku tozo nyingine 54 zikiwa zinahusu Biashara.

Serikali imepanga kuendelea kufanya mageuzi ya sheria, kanuni, tozo na utendaji wa sekta ya umma ili kuvutia sekta binafsi katika uwekezaji. Hivyo basi, tutarajie ubora zaidi katika kipindi hiki cha miaka mitano ijayo.

**Kuondoa Urasimu :**
**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Vilevile, ili kuvutia wawekezaji wengi kwenye viwanda, serikali imejipanga kujenga mazingira rafiki kwa wawekezaji mazingira tunayoyaweka kama vile miundombinu, umeme, maji, Rushwa na kuondoa vikwazo visivyo vya lazima kama vile urasimu uliopitiliza. Natumaini mnakumbuka, Mheshimiwa Rais alipokuwa akilihutubia Bunge mnamo tarehe 13 Novemba 2020, pamoja na mambo mengine alitoa msimamo wa serikali kwamba kuanzia sasa anataka Wawekezaji wanapokuja nchini wapatiwe vibali vya kuwekeza ndani ya siku 14.

Aidha, nitumie fursa hii kuwataka viongozi wote wanaohusika kuhakikisha wanafanya kazi kwa karibu na waajiri wote hususani wa sekta binafsi ilikujenga mazingira rafiki kwa ukuaji wa Biashara na uwekezaji nchini.**Kwa pamoja inawezekana!**

**Kukuza na Kuimarisha Sekta Binafsi:**
**Mheshimiwa Mwenyekiti,** itakumbukwa kwamba, tarehe 13 Novemba 2020 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika hotuba yake ya ufunguzi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jijini Dodoma alisisitiza kutoa Kipaumbele kwa Sekta Binafsi katika kipindi hiki cha pili cha Serikali ya Awamu ya Tano. Naomba ninukuus ehemu ya hotuba yake.

> "…**Muhimu zaidi ni kwamba katika kipindi hiki cha miaka hii mitano ijayo ya utawala wangu Sekta Binafsi itapewa umuhimu wa kipekee sana. Tunataka mtu yeyote atakayetaka kuwekeza asisumbuliwe kwa kuwekewa vikwazo vya aina yoyote,"**

Kauli hii ya Rais wetu mpendwa inaonesha utayari wa serikali kuiboresha shughuli za uwekezaji nchini.

**Migogoro ya kibiashara:**
**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali iko tayari kujadiliana na Sekta binafsi ili kutafuta muafaka wa migogoro ya kibiashara (Business Disputes) iliyopo kwa faida ya pande zote mbili lengo likiwa ni kuona Tanzania inakuwa sehemu salama zaidi ya kufanya biashara duniani. Hivyo natumia fursa hii kusisitiza kwamba serikali yetu imejipanga kikamilifu kuhakikisha inaendelea na utaratibu huo ili kukuza biashara na uwekezaji hatimaye kuongeza fursa za ajira nchini.

**Tozo ya kukuza Ujuzi :**
**Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabibi na Mabwana**,
Natambua umuhimu na uhitaji wa kupunguza tozo inayolipwa na waajiri kwa ajili ya kukuza ujuzi mahali pa kazi maarufu kama '**Skills and Development Levy (SDL)'** ambayo kwa sasa tumeipunguza hadi asilimia 4.0%.

Ikumbukwe kuwa tozo hii imekuwa ikipungua hatua kwa hatua kutoka asilimia 6% mpaka asilimia 5% (2014) na asilimia 4.5% na mwaka huu wa fedha imepungua mpaka asilimia 4.0%. Kama sehemu ya jitihada za kupunguza gharama ya uwekezaji nchini, serikali inakaribisha ushauri kutoka kwa waajiri na wadau mbalimbali kuhusu namna tunavyoweza kuziba pengo kutokana na mapendekezo ya waajiri kutaka tozo hii ishuke mpaka asilimia mbili.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwaniaba ya Serikali nawakaribisha wawekezaji wa ndani na wale wa kutoka nje ya nchi waje kuwekeza katika sekta mbalimbali kwa manufaa yetu sote. Sisi tupo tayari kuendelea kufanya kazi na sekta binafsi hasa kupitia ATE ambayo kimsingi husaidia kutoa ushauri na uwakilishi katika maeneo ya sheria za kazi ikiwemo kutoa mafunzo mahali pa kazi. Napenda niwahakikishie wadau wa sekta binafsi kuwa Tanzania ni mahali pazuri na sahihi pa kuwekeza na ni nchi yenye amani na utulivu.

Licha ya hayo pia tumebarikiwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji hasa katika maeneo ya kimkakati likiwemo eneo la mafuta na gesi, viwanda, vivutio vya utalii, kilimo na ufugaji. Nchi yetu pia ni Mwanachama wa jumuiya mbili za kikanda, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Jumuiya hizi zitumike kama fursa kwani zina soko la watu takriban milioni 500.

**PROGRAMU ZA KUINUA FURSA SAWA KWA WOTE**
**Mheshimiwa Mwenyekiti,** natambua pia umuhimu wa kujenga uchumi wenye manufaa kwa watu wote hususani watu wenye ulemavu. Natambua kazi nzuri inayofanywa na ATE kupitia Mradi Jumuishi kwa Wote (All Inclusive Project) kwa kushirikiana na CEFA NGO kutoka nchini Italia, CCBRT na wadau wengine unaolenga pamoja na mambo mengine, kuboresha afya na hali ya kiuchumi kwa watu wenye ulemavu katika Jiji la Dar es Salaam.

Hivyo, natumia fursa hii kuwasisitiza waajiri wote nchini kuwa tayari kuwapokea na kuwapa ushirikiano Watu wenye ulemavu ili waweze kupata fursa ya kuchangia katika shughuli za ujenzi wa Taifa kama Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini inavyotutaka.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** nitumie fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru ATE kwa kuunga mkono Serikali katika kuhakikisha nchi yetu inakuwa na uwiano mzuri wa kijinsia hasa katika nafasi ya uongozi. Nimefarijika sana kusikia mnatekeleza mpango mzuri wa mafunzo chini ya programu ya Mwanamke Kiongozi (Female Future Program). Nimeelezwa kuwa

mmekuwamkifanya mafunzo kwa wanawake kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Waajiri nchini Norway (NHO) kwa lengo kuwawezesha wanawake kushika nafasi za juu za uongozi katika makampuni na taasisi mbalimbali ambapo nimetaarifiwa kuwa tangu kuanza kwa programu hii mwaka 2016 mpaka sasa jumla ya wanawake 150 wamekwishahitimu mafunzo hayo.

Pongezi nyingi nazituma kwa kampuni ambazo zimefanikisha kuleta wafanyakazi wao katika programu hii yenye lengo la kuwajengea uwezo wanawake kwa ajili ya nafasi za juu za uongozi na kuwapa uwezo wa kuingia kwenye Bodi mbalimbali na kushiriki katika kutoa maamuzi.

Ni jambo la kujivunia kuwa baadhi ya wanawake waliohitimu tayari wamefanikiwa kupata nafasi za juu za Uongozi na pia kuwawakilisha kwenye Bodi mbalimbali huku mchango wao ukionekana dhahiri.

Vilevile, ninashukuru ILO, Shirikisho la Vyama vya Waajiri nchini Norway (NHO) na Shirika la CEFA NGO kutoka Italia, CCBRT na wadai wengine wote wanaoshirikiana na ATE katika kuunga mkono jitihada za Serikali kuwafikia Watanzania na makundi maalum ya wanawake na watu wenye ulemavu.

Nipende kutoa rai yangu kwa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), taasisi mbalimbali za kibiashara na wadau mbalimbali nchini waunganisha nguvu nakuhakikisha Programu hii inakuwa endelevu kwa kuwahamasisha wanawake wengi zaidi kushirikimafunzo haya. Kwa kuwa baada ya hotuba yangu mtaendelea na majadiliano, ni matumaini yangu yale mtakayoyojadili na kutoa ushauri na tuupate.

**MAELEKEZO NA MASUALA YA MSISITIZO**

Ndugu washiriki wa mkutano na viongozi mbalimbali, napenda kutumia nafasi hii kutoa msisitizo na maagizo yafuatayo kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji;

i. **Mafunzo ya urasimishaji ujuzi (Uanagenzi):** kutokana na uboreshaji wa sekta ya elimu, kumekuwa na ongezeko, kubwa la wahitimu katika ngazi mbalimbali. Vijana hawa wanaohitimu katika vyuo vya elimu ya juu, vyuo vya elimu ya kati pamoja na vyuo vya ufundi wanahitaji kupitia hatua ya mafunzo mahala pa kazi ili kuwa na ujuzi stahiki wa kuweza kuajiriwa. Ninawapongeza sana waajiri wote nchini ambao wamekuwa mstari wa mbele kutoa fursa ya mafunzo mahali pa kazi kwa vijana wetu wanaohitimu vyuo. Msisitizo wangu kwa waajiri ni kuwa wote tutoe kipaumbele **cha kutekeleza** mpango huu wa mafunzo mahala pa kazi kwa vijana wetu ili kuwapa maarifa, ujuzi na uwezo unaofaa katika soko la ajira.

ii. **Afya na Usalama mahala pa kazi**: Wafanyakazi ndio nguvu kazi na mtaji namba moja katika uzalishaji mali hivyo, waajiri wote hakikishenimnazingatia sheria Na.5 ya mwaka 2003 kuhusu afya na usalama mahala pa kazi kwa kusajili maeneo yao ya kazi ili Mamlaka husika ikiwemo OSHA ziweze kutoa ushauri na namna ya kuwalinda wafanyakazi na uwekezaji wenu.

iii. **Maslahi ya watumishi**: Ninazo taarifa za kuwepo waajiri ambao wanadaiwa malimbikizo ya michango na adhabu jambo ambalo husababisha mateso na usumbufu katika ulipaji wa mafao kwa watumishi wengi wanapostaafu. Ninawagiza waajiri wote

kujali maslahi ya watumishi kwa kuwasilisha michango ya watumishi katika mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wakati na kwa usahihi.

iv. **Vyama vya Wafanyakazi mahala pa kazi:** baadhi ya Waajiri wamekuwa na tabia ya kuwanyima wafanyakazi fursa ya kuanzisha vyama vya wafanyakazi mahali pa kazi. Wafanyakazi wanaambiwa chagua moja chama au ajira na maeneo wanaporuhusiwa wakimaliza mikataba yao wanazuiwa kuongeza mikataba. Hivyo nawaagiza waajiri wote kuwa Wafanyakazi waruhusiwe kuanzisha na kujiunga na vyama vya Wafanyakazi mahali pa kazi kwa kuzingatia sheria za kazi.

**v.** **Mikataba ya Ajira:** Waajiri wengi wanatumia utaratibu wa *outsourcing* hivyo wafanyakazi wengi kuishia kuwa na kazi za muda (casual employees). Utaratibu huu unawanyima wafanyakazi kupata haki zao kama mafao ya NSSF, WCF nk. Hivyo ninasisitiza waajiri wote kuzingatia kutoa mikataba ya ajira kwa wafanyakazi ili kufikia dhana ya kazi zenye staha **(decent work).**

**vi.** **Soko la ajira la ndani:** tatizo la ajira lipo duniani kote**,** kumekuwepo mwenendo wa baadhi ya Waajiri kupendelea kutoa ajira kwa raia wa kigeni hata kwa nafasi ambazo zingeweza kujazwa na soko la ajira la ndani. Sambamba na hilo, kumekuwa na ongezeko kubwa la kuomba nyongeza ya muda zaidi ya uliowekwa kisheria kwa wafanyakazi wa kigeni kufanya kazi nchini. Hali hii inawanyima fursa za ajira wazawa wenye sifa na nafasi hizo kuchukuliwa na wageni. Hivyo, nawaagiza waajiri kuwekakipaumbele cha kuajiri wazawa wenye taaluma na ujuzi stahiki kujaza nafasi mbalimbali za kazi.

Pia waajiri watekeleze mipango ya mafunzo kupitisha ujuzi kwa wafanyakazi wao ili kuwajengea uwezo wafanyakazi wazawa kushika nafasi mbalimbali zinashikiliwa na wageni pindi muda wao wa kufanya kazi nchini unapokwisha.

**vii.** **Mahitaji ya ujuzi kwenye soko:** ili kufikia malengo katika uzalishaji na uwekezaji**,** Waajiri mnayo fursa ya kushirikiana na Serikali ili kuanisha mahitaji ya aina ya ujuzi mnaoutaka katika maeneo yanu ya kazi. Hii itaiwezesha Serikali kutoa mafunzo ya kukuza ujuzi unaoendana na mahitaji mliyonayo. Kwa kufanya hivyo tutaendelea kukuza soko la ndani la ajira.

**viii.** **Kulipa Kodi:**Nchi yetu imeendelea kushirikiana na waajiri kutoka sekta zote, Vyama vya Wafanyakazi na wananchi kwa ujumla ili kutimiza azma ya nchi yetu kujitegemea. Ili dhana hii iweze kuwa halisia ; ninawasihi wote tuunge mkono jitihada za Serikali kwa kulipa kodi zetu kikamilifu.hii ndio njia pekee ya kulifanya Taifa letu kujitegemea.

**MWISHO**

**Mheshimiwa Mwenyekiti Mabibi na Mabwana**,

Wakati nikihitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kuwapongeza waajiri na Watanzania wote kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali yetu inayoongozwa na **Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe JosephMagufuli** katika vita dhidi ya ufisadi na vitendo vya rushwa ambayo kimsingi imesaidia kuleta mageuzi na fedha ambazo zimekuwa zikiokolewa

kutokana na vita hiyo tunaendelea kuzielekeza katika kutoa huduma kwa wananchi kupitia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Mwenyekit**i, ni ukweli usiopingika kuwa sekta ya viwanda imekuwa ikitoa ajira nyingi na na duniani kote na imekuwa ndio muhimili mkuu wa ukuzaji uchumi na nyenzo kuu ya kupambana na umasikini. Serikali kwa kutambua hilo imejipanga kushughulikia changamoto ya ajira nchini kwa kuimarisha na kukuza sekta ya viwanda nchini huku mkazo mkubwa tukiuweka kwenye viwanda venye kuzalisha kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini pamoja na kuongeza thamani ya mazao yanayolimwa nchini badala ya kuuza malighafi.

**Mwisho,** ninawapongeza tena ATE kwa kufikisha umri huu wa miaka 60 tangu kuanzishwa kwake na kipekee zaidi niwashukuru kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa Mgeni rasmi katika tukio hili la kihistoria ambalo hakika limependeza na kufana sana. Zaidi ya yote nawapongeza waajiri wote kwa kuendelea kuwa wanachama wazuri katika chama chenu hiki cha waajiri ambacho ndio chombo pekee cha waajiri kinachowawakilisha vema nchini Tanzania chenye lengo la kuwakilisha na kutetea maslai ya waajiri nchini katika masuala ya kazi na ajira.

Nitoe wito kwa waajiri wotekuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha masuala mbalimbali yanayohusiana na biashara na uwekezaji yanapata ufumbuzi kwa manufaa ya ukuaji wa uchumi wetu.

Kwa kuwa leo nipo na waajiri ambao mna waajiriwa wenu, wako walio wengi wanaajiriwa kwenye Serikali na waliojiajiri kwenye sekta mbalimbali Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Biashara mbalimbali na yeyete aliyapo nchini.

Natumia nafasi hii kuujulisha **UMMA** wa Watanzania kuwa sikukuu ya Uhuru ya mwaka huu wa 2020 hatutasherekea kwa kukusanyika pamoja na kuona maenesho na kusikiliza hotuba za viongozi. Badala yake kila Mtanzania atajishuhulisha na shughuli za kiuchumi.

**MUNGU IBARIKI ATE,**
**MUNGU IBARIKI TANZANIA**
**Asanteni sana kwa kunisikiliza**!